

4.- الشَّفَّاتُ Ash-Shafataan - Midomo miwili:

Kunapatikana makhraj mbili inayotoa herufi nne:

- i) Kutoka katika tumbo la mdomo wa chini na meno ya mbele ya **juu** inatoka herufi ya **ف**
- ii) Midomo miwili yote inapofungwa; pamoja na kushirikishwa na pua (khayshuwm) inatoka herufi ya **م**.
Midomo miwili yote inapofungwa mfungo wa nguvu hutoka herufi ya **ب**.
Herufi ya **و** isiyokuwa ya madd inatoka kwa kukusanyika midomo yote miwili mbele pamoja na kubakia uwazi wenyе kutoka sauti ndani yake.

5. الْخَيْشُومُ Al-Khayshuwm - Puani

Ni sehemu iliyopo ndani ya pua na pia husemwa kuwa ni uwazi ambao unaunganisha baina ya pua na mdomo, hutoka ndani yake makhraj moja tu nayo ni al-ghunnah.

Tanbihi: Ghunnah sio herufi bali ni Swiffah inayohusu herufi za **هـ** na **نـ** ni sauti inayotoka katika pua ambayo haina uhusiano na ulimi.